# Kwamini ualalishaji wa utoaji wa mamba si mzuri kwa afya ya Mwanamke



UTHIBITISHO UNOANYESHA YA KWAMBA utoaji mimba aupunguzi vifo vya wamawate wajanazito.

Waasisi wa ualalishaji wa utoaji mimba wanadai yakwamba sheria zilizowekwa kuzuia utoaji wa mimba usababisha vifo vya wanawake wengi wanatoa mimba kwa njia hatari zisizo halali. Madai haya ni kinyume na uthibitisho ulimwernguni kote. Vifo vya wajawazito hutegemeana kwa ukubwa na huduma za afya zipatikanazo katika vituo vya afya na sio ualalishaji wa miomba au kuwepo kwa utoaji wa mimba.

Ualalishaji wa utoaji wa minba kwa hakika huatarisha maisha ya mwananke kwa njia nyingi na pia kuvunja sheria za haki za mwanadamu.


## Shida na vifo vya wajawazito.

Kulingana na somo lalilochapishva mwaka wa 2010 na gazeti moja la afya “The Lancet”, linaonyesha vifo vya kutokana na hali za wajawazito zilipungua hadi asilimia 35 kutoka mwaka 1980 hadi 2008.[1] Mchakato huu umekubalika na ni muhimu lakini vifo vya wajawazito vimebakia katika kiwango kilekile cha kupuuzwa katika nchi zinazoendelea (nchi maskini).

Katika mambo mengi hasa mahitaji muhimu ya kiafya katika jamii yanaupungufu. Mara nyingi hakuna mkunga na mazingira ya vituo vya afya ni hayaridhishi kiusafi. Vifaa muhimu na vya ziada vya kutoa huduma ya papohapo kama gari la kukimbiza wagonjwa kutoka kituo kimoja kwenda kingine kwa ajili ya matibabu bora havijitosdhelezi, na mara nyingine kukosa kabisa. Madaktari hawajafundishwa na kufuzu mafunzo ya uganga na ukunga na hata kutoa huduma nyingine muhimu za afya. Mbali na hayo vifaa hivyo kuwa adimu na kukosa kabisa pia limechangia kwa ukubwa zaidi huduma hizi kuwa mbaya (Hatari katika mwanamke mjanzito ipo tu hata kama mimba inasitishwa kwa kutolewa au kuzaliwa mtoto).

## Njia na suruhuhisho kushinda/Jawabu;

Vifo vya waja wazito wengi vinaweza kupunguzwa kwa kuwepo utoshelezi wa vyakula vyenye vitamini kwa kina mama, huduma muhimu za afya na huduma bora za mkunga kwa mzazi pindi ana mimba, pindi anajifungua na hata baada ya kujifungua.




Sehemu. 1

Katika nchi zilizoendelea kiwango cha kupunguzaa vifo vya wajawazito vinalingana na viwango vya huduma na utaalamu wa wakunga waliofuzu mafunzo kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wajawazito. (kutoka mwaka 1935 hadi 1950), Shirika kuu la afya duniani (WHO).[2] Hili lilianzishwa vizuri kabla ya kuenea kwa ualarishaji wautoaji mimba.

**Katika umoja wa mataifa, utoaji wa mimba kwa kiasi ulikuwa wa kawaida (Haukutishia maisha ya mzazi). Utoaji wa mimba ulialalishwa mapema mwaka 1973 (angalia uk 1). DK. Mary Calderone, Mwaka 1960, Mkuregenzi wa kale wa huduma za afya za uzazi, alisema kwamba utoaji wa mimba sio hatari tena kwa kuwa unafanywa vizuri na kwa utaalamu wa hali ya juu na waganga waliofuzu mafunzo.**[3]

DK. Bernard Nathanson wa kale, na mwanzilishi wa utoaji sera za utoaji mimba wa NAPAL pro-choice huko America, Mwaka 1973, Aliandika kwamba, sera ya malalamiko kuwa wanawake wangelikufa kutokana na hatari za utoaji wa mimba usio kubalika katika umoja wa mataifa, “sasa sera hiyo haitumiki tena, Antibayotiki na madawa mengine yameleta punguzo kubwa katika idadi ya vifo vya wajawazito.[4]

Uingereza na Ughaibuni uwiana kwa vifo vya wajawazito (UVW), idadi ya vifo vya wajawazito kwa 100,000 wanaozaliwa iliporomoka zaidi ya 550 katika mwaka 1931 hadi kufikia 50 katika mwaka 1960. Maporomoko hayo yanalingana na viwango vilivyopo vya huduma na madawa katika wajawazito.[5]

Maleysia na srilanka wamepuguza kwa ukubwa vifo vya wajawazito kwa kutoa mafunzo ya wakunga, viongozi na madaktari na manesi kwa upana katika vijiji na sehemu ambazo zina maendeleo ya chini, na kuhakikisha kuwepo kwa usambazaji bora wa madawa na vifaa vya matibabu, kuzingatia kuwepo kwa huduma bora na za haraka za usafiri na mawasiliano na hasahasa huduma za ziada za haraka.[6]

**Kupunguza vifo vya wajawazito, tunatakiwa kuweka juhudi katika kumpatia mwanamke wa nchi ambazo zinaendelea uwezo sawa wa huduma bora, kama mwanamke wa nchi zilizoendelea kila mara ambazo zitaboresha afya ya mama na motto.**

## Ualalisho aumanishi usalama.

Kinyume na malalamiko ya mashirika yanayounga mkono utoaji wa mimba salama, Hakuma Mawasiliano ya moja kwa moja kati ya swala la utoaji salama wa mimba na kiwango cha vifo vya wajawazito. Kwa hakika utoaji wa mimba unaweza kukubalika lakini sio salama kwa mwanamke na unaweza kuwa mbaya, lakini! kwa kiasi kidogo ni salama. (Angalia uk. 2).

Kutokana na Makadilio ya shirika la afya duniani, shirika la wakimbizi, shirika la UNFPA na benki ya kimataifa, Nchi nne ambazo zimepunguza kiwango cha vifo vya wajawazito kati ya kipindi 1990 na 2008 ni Maldives, Romania, Iran na Bhitan.[7] Nchi tatu kati ya hizo (Ukitoa Romania) zimezingatia sheria yao juu ya utoaji wa mimba.


**Mipango mingine mingi inaonyesha kupinga kwamba mchakato wa utoaji mimba hauongezi vifo vya wajawazito. Mwaka 1989, Chile walipinga utoaji wa mimba, na idadi ya vifo ilizidi kupungua. Leo hii chile inakumbwa na idadi ya asilimia kidogo sana za vifo katika mataifa ya Amerika na ukizingatia utoaji wa mimba haukubaliki.**[8]

Katika mataifa ya marekani ya kati ya Nicaragua na £L-salvador, Utoaji wa mimba ni haramu kabisa. Nicaragua imeshuhudia kiwango cha vifo vya wajawazito kimepungua kwa asilimia 44 kutoka mwaka 1990; kiwango cha vifo vya wajawazito cha EL-salvador nacho kimepungua kwa asilimia 44.[9]

Uolanzi wamekataza utoaji wa mamba na kuzusha wanachoamini watu wengi kuwa ndio wenye vifo vichache vya wajawazito.[10] Polandi walikataza utoaji wa mimba mwaka 1993, baada ya maka anbayo utoaji wa mimba uliendekezwa sana. Huko Polandi vifo vya wajawazito vimepungua kwa kiasi cha

asilimia 67, tangu mwaka 1990, na ni miongoni mwa nchi zilizo na kiwango kidogo cha vifo vya aina hiyo ulimwenguni.[11]

**Ukweli ni kwamba Afrika kusini walipenda kuipitisha na kuikubali sera ya utoaji mimba katika mwaka wa 1997. Tangu siku hizo vifo vya wajawazito viliongezeka. Sasa vifo vya wajawazito vimekadiliwa kufikia hadi 410, karibu kufikia kiwanfo cha mwaka 1990[12] cha kule kanada; ampapo wanaruhusu utoaji wa mimba na kuleta angezeko la asilimia 94 kutoka mwaka 1990 hadi 2008.[13] Vifo vya vya wajawazito katika mataifa ya Narekani ambapo pia wanaruhusu utoaji wa mimba vimeongezeka kwa asilimia 96.[14]**




Chimbuko: shirika la afya Duniani na mengineyo, Mabadiliko katika vifo vya wajawazito katika mwaka 1990 na 2008.

Sehemu. 2

## Uhalalishaji wa utoaji mimba hujenga mazoea

Ualalishaji wa utoaji mimba sasa unaonekana jambo la kawaida katika baadhi ya nchi. Kuruhusu utoaji wa mimba haumaanishi kwamba mchakato huo kuwa salama, hizi ni imani potofu. Huko Marekani ambapo wamehalalisha utoji wa mimba mchakato huu umeleta ongezeko kubwa la utoaji mwingi wa mimba. Katika umoja wa mataifa wa Marekani imekadiliwa utoaji wa mimba kufikia 98,000 kwa mwaka, na hata kufikia kilele cha idadi ya million 1.6 kwa mwaka wa 1973,[15] tangu wakati huo zaidi ya watu Million 53 wametoa mimba.[16] Stanley Henshaw wa chuo cha Gehmacher (Mwakilishi) Anaeleza kuwa katika nchi nyingi utoaji wa mimba ulipo alalishwa umekua jambo la kawaida kama ule tu wa marekani ulio endekezwa zaidi na hata kufikia kukubalika.[17]

**Tunawezaje kupunguza vifo vya wajawazito kwa watoto?**

- Tunatakiwa kutumia asilimali zetu ili kusaidia huduma za afya katika zinazotumika na wanawake na mabinti.
- Tunatakiwa kijitahidi kuwapatia wanawake wa nchi zinazoendelea uwezo sawa na ule ule anaopewa mwanamke katika nchi zilizoendelea kwa kila baada ya mda, Ili kuhakikisha tunaweza kuleta maendeleo ya afya kwa mama na mtoto.

## Kitu haki hupendelea

Utoaji wa mimba ulioalalishwa hausaidi chochote katika kutatua tatizo la uduma maskini za afya katika nchi zinazoendelea. Na hivyo basi kuna angalau baadhi ya sababu kuu tatu nzuri ambazo kwanini chaguo la utoaji mimba si jema.

**Kwanza**, Haki huitaji serikalki kutunza sheria muhimu za kila mtu katika jamii. Ukweli wa sayansi uliositirika unadai yakwamba mtoto ambaye hajazaliwa ni kumbe hai na kinaishi (*hamo sapiens*). Kama vile tu ilivyo kwa kila mmoja wetu, kwanzia siku ya kwanza ya ukuaji wake tumboni.[18] Hivyo ni sheria iliyojengwa na umoja wa mataifa katka haki za binadamu[19] kwamba watu wote wana haki sawa katika misingi ya haki kwa jamii na wanaitaji kuheshimiwa na kulindwa.[20] Hivyo sheria inatakiwa kuwalinda Malkia watoto na vichanga ambao hawajazaliwa kama vile tu sheria inavyotulinda sisi ambao tumeishazaliwa na kuwa watu wazima. Na kumbuka hata sisi tulipitia hatua hiyohiyo , hivyo hatuna budi kuwalinda vichanga. Sheria yoyote ambayo inaruhusu uuaji wa viumbe kama hao ni haramu, na hatua kali inapaswa kuchukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.

**Pili**, kwa sababu ualalishaji wa utoaji mimba kwa kawaida unaongeza idadi kubwa zaidi ya utoaji mimba, pia uongeza idadi ya malikia (vichanga) ambao hawana dhambi (walio tumboni) kufa kwa zaidi. Kiwango hicho cha mauaji kimefanya utoaji wa mimba kuwa wa kawaida na kuonekana cha haki katika nchi ambazo wamehalalisha jambo hili. Maisha ya watu yanapotea, pindi utoaji wa mimba unapohalalishwa.

## Hatari ya utoaji mimba

**Tatu**, utoaji mimba hata nchi ambazo zina uduma na ubora wa vituo vya afya kama Umoja wa Mataifa wa Marekani wanawake wapo katika sehemu kubwa ya hatari.[21] Uwezekano wa upasuaji wa sehemu za mwili (Oparesheni) katika sehemu za uzazi za mwanamke, inaweza kusababisha uaribifu wa mimba, na hata kuleta maumivu makali, na hata kukomesha uzazi kabisa.

**Mda mwingine utoaji wa mimba ni mgumu sana ambao unaweza sababisha kifo kwa mama mjamzito. Zaidi ya wajawazito 400, huko Marekani wamepoteza maisha tangu mwaka 1973 kutokana na utoaji mimba uliohalalishwa.[22] Madhara makubwa yanayotokea baada ya utoaji mimba ni kama, kujifungua mimba changa, kupata kansa ya matiti na hata kukoma uzazi kabisa, pia mtoto kujitunga nje ya tumbo la uzazi, hii yaweza kusababisha maafa kama matibabu bora na ya haraka hayatazingatiwa mapema.**

Utoaji na mimba pia unaweza kuleta madhara mengine wengi kama, huzuni, kudhuhurika na madawa vibaya, kuwa na mawazo yasababishayo kutopata usingizi na hata kuleta ugonvi (kutoelewena) baina ya wapenzi na jamii nzima, na pia imetela majuto makubwa kwa wake na waume kwa kushiriki tendo hili la utoaji mimba.[23]

Utoaji wa mimba katika nchi ambazo hazijitosherezi kimadawa na huduma bora moja kwa moja hii ni hatari katika nchi hiyo na italeta matatizo na mateso mengi kwa wanawake na hata baadae kuleta vifo vingi. **Jeanne E. Head, R.N, Mwakilishi kutoka Umoja wa Kimataifa katika kitengo cha haki ya kuishi, Anaelezea, "wanawake wapo katika hatari kwa sababu wanakosa kumwona daktari (kuhudhuria kliniki ya wajawazito), kwenda hospitali au kupata madawa kabla ya kuruhusiwa kufanya utoaji huo wa mimba uliohalalishwa, na**

**Sheria za kimataifa zinamgundua na kumtambua mtoto aliye haribiwa (kutolewa kutoka tumboni).**

**«Mtoto kwa jinsi ya mwili na Akili changa anahitaji ulinzi muhimu na huduma bora ukizingatia ulinzi uliositirika kabla na baada ya kujifungua kwa mama.»**

***Sheria inayo mlinda mtoto***

**«Ugunduzi wa tabia hizo na huduma zisizo za haki kwa wahusika imekua msingi bora wa uhuru, na haki dumiani.»**

***Sheria inayo mlinda binadamu***

**mtu kama huyu atakua hatarini hata baada ya kuruhusiwa kufanya utoaji huo wa mimba.**

Na kama uhalalisho wa utoaji mimba utapendwa na watu wengi basi kama ilivyo katika nchi nyingine nyingi madhara na hatari kubwa zitawapata wale wanao ogopa huduma zilizo bora zipatikanazo hospitali.[24]

## Mwanamke anahitaji matunzo muhimu

Utoaji mimba uliohalalishua unaleta idadi la ongezeko kubwa la utoaji mimba hivyo utoaji huu pia huusisha madhara mengi kwa mwanamke. Huduma bora katika vituo vya afya tu, ndio vinavyoweza kuleta suruhisho katika vifo vingi vya wajawazito kwa watoto katika nchi zinazoendelea (Maskini).

---

Vielelezo,


1. Margaret C. Hogan, et al., vifo vya watoto na wajawazito kwa nchi 180, katika miaka ya 1980-2008: Mchakato unaendelea kufikia malengo endelevu ya karne 5. "The Lancet" 375, 9726 (8 May 2010): 1609-1623.
2. Shirika la afya Dumani, vifo vya wajawazito kwa watoto, kitabu cha ukweli duniani ( Sheria ya makubaliano ya shirika la afya dumiani 1991).
3. Mary S. Calderone, Utoaji wa mimba usio halali ni tatizo kubwa la afya "vituo 50 vya afya vya marekani (Julai 1960): 949.
4. Bernard N. Nathanson na Richard N. Osuing, Utoaji mimba Marekani (New York Doubleday, 1979): 194.
5. Shirika la Afya Duniani, vifo vya wajawazito kwa watoto: Kitabu cha ukweli duniani.
6. Benki ya Dunia, Ripoti ya maendeleo duniani 2006 (Julai 2004).
7. Shirika la Afya Duniani na mengineyo. Natawi katika vifo vya wajawazito kwa watoto: 1990 hadi 2008 (sheria dhidi ya makubaliano ya shirika la afya duniani mwaka 2010), 33.
8. Hogan na wengineo.
9. Shirika la afya duniani na mengineyo, matawi katika vifo vya wajawazito kwa watoto; 29, 30.
10. 29 (kitabu hicho hicho).
11. 31 (Kitabu hicho hicho).
12. Angalia Tena, Raia wa Minnesota wahusikao na ziara za Kimaisha duniani, Jinsi Africa ya kusini inavyowapoteza wanawake kwa watoto. (Minneapolis: MCCL, 2011); inapatikana katika http://www.mccl-go.org/resources.htm.
13. Shirika la afya na mengineyo, Matawi katika vifo vya wajawazito kwa watoto, 28.
14. Katka kitabu hicho hicho 32.
15. Kikundi cha utafiti mwaka 1981, walikadilia wastani wa 98,000 wa utoaji wa mimba usio alalishwa kwa kila mwaka katika kipindi cha miaka 32 kabla ya ualalisho wa utoaji mimba. Barbara J. Syska, Thomas W. Hiloers, MD, and Dennis O' Hare "kitengo cha kuhusika na kesi za utoaji mimba na Madhara yake kwa kutumia sheria ilikowekwa na jamii". Katika mwonekano mpya wa utoaji mimba, na mengineyo, Thomas W. Hiloers, MD, Denis J. Horan na David Mall (Frederick, MD: University Publications of America, 1981).
16. Angalia http://www.nrlc.org/Factsheets/FS03_AbortionInTheUS.pdf.
17. Stanley Henshaw, Guttmacher Institute (16/06/1994) ulitolewa rasmi.
18. Kwa mfano, Angalia, Robert P. George na Christopher Tollefsen, Embryo: Ulinzi katika maisha ya binadamu (New York: Doubleday, 2008); na Maureen L. Condic, "ni lini maisha ya mwanadamu yanapoanza? Kama sayanzi ilivyo", Westchester Institute White Paper Series (Mwezi wa kumi mwaka 2008), inapatikana katika http://www.westchesterinstitute.net/images/wi_whitepaper_life_print.pdf.
19. Usemi rasmi (utambuzi wa tatizo hilo na sheria zisizo za haki katika jami ndio chanzo cha uhuru, haki na Amani duniani), "Inasema kwamba kwa mtu yeyote anayo haki ya kuishi, kuwa huru na kujihami".
20. Kwa ulinzi wa sehemu hii, angalia Francis J. Beckwith, kutetea maisha Tabia na taratibu za kisheria zinazopinga chaguo la utoaji mimba. (New York: Cambridge, 2007); Patric Lee, utoaji mimba na zisizofikia kutolewa, Toleo la pili (Washington, D.C.: Jarada la Chuo kikuu cha Roma Marekani, 2010); na Christopher Kaczor, Sheria za utoaji mimba: Haki ya mwanamke, Maisha ya mwanadamu na maswali ya haki (New York: Routledge, 2011).
21. Kwa mfano, Anglia, Elizabeth Ring-Cassidy and Ian Gentles, Afya ya wanawake baada ya utoaji wa mimba. Matibabu na ushaidi wa mwonekano wa kiakili, Toleo la pili (Toronto: The deVeber Institute, 2003).
22. Shirika-la kupingana na magonjwa na litoalo kinga, "Watafiti wa utoaji mimba, Umoja wa mataifa marekani, 2007" Ripoti sitini za huzuni kwa kila wiki, Namba moja (25/02/2011).
23. Angalia kwa mfano, http://www.afterabortion.org.
24. Jeanne E. Head and Laura Hussey, "Je utoaji wa mamba unasaidia afya ya mwanamke?" Dunia na mimi, mwezi wa sita mwaka 2004, 56.



MCCLGO! GLOBAL OUTREACH

**Wazalendo wa Minnesota wahusikao na ziara ulimwenguni kwa kupigania haki za maisha ya watu**

4249 Nicollet Avenue | Minneapolis MN 55409 USA

612.825.6831 | Fax 612.825.5527

MCCL@mccl.org | **www.mccl-go.org** | www.mccl.org


Nakala hizi hupatikana pia katika lugha ya kispanishi na kifaransa tafuta katika tovuti hii www.mccl-go.org au omba nunua nakala yakokupitia tovuti hii MCCL@mccl.org


Imeandaliwa na Umoja wa Mataifa Marekani



© 2011 MCCL



national RIGHT TO LIFE Educational Trust Fund

**Mfuko wa elimu na haki za kuishi za kimataifa**

211 East 43rd Street, Suite 905 | New York, NY 10017 USA

212.947.2692

NRLC@nrlc.org | **www.nrlc.org**


Mfuko wa elimu na haki za kuishi za kimataifa
ni shirika la kujitegemea la kimataifa (pro-life NGO).


Photo: Bread for the World